# TAARIFA YA MWAKA- 2020/2021

**MAMAS' HOPE (MHOLA)**
**ORGANIZATION FOR LEGAL ASSISTANCE**



Picha 1: Wafanyakazi kutoka H3000 na MHOLA walipotembela mojawapo ya Kikundi kinachofadhiliwa na MHOLA

**Imeandaliwa na:**

**Saulo P. Malauri – Mkurugenzi**

**November, 2021**

## WADAU WA SHUGHULI ZA MHOLA

VEREIN ZUR | ANITA FOUNDATION

LSF Legal Services Facility · Better Way Foundation · HORIZONT3000 · With funding from Austrian Development Cooperation · Katholische Frauenbewegung · schwelle Foundation Contributions to Peace

# YALIYOMO

**Taarifa** **Ukurasa**

**Shukrani ……………………………………………………………………….2**

**Kuhusu MHOLA……………………………………………………………….3**

**Malengo, Shughuli, Mafanikio……………………………………………….4**

**Vyanzo vya mapato…………………………………………………………11**

**Funzo katika utekelezaji……………………………………………………11**

**Changamoto …………………………………………………………………11**

**Malengo ya 2021/2022………………………………………………………12**

## SHUKRANI

Ni heshima kubwa kuitaja serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, marafiki na wadau wetu wakuu ambao ni Better Way Foundation (USA), Austria Development Cooperation, Kfb, H3000, Threshold foundation(D), Anitha Foundation, Wizara ya katiba na Sheria na Kituo cha Malezi MHOLA DAY CARE, vyombo vya Habari na jamii nzima ya Mkoa wa Kagera kwa mchango wao mkubwa wa fedha na utaaram katika kufanikisha utendaji wa kazi nzuri ya MHOLA kwa mwaka 2020/2021.

Aidha shukrani za pekee kwa wajumbe wa Bodi ya MHOLA kwa kuwa bega kwa bega na wafanyakazi wa MHOLA na hasa ktika kipindi hiki kigumu cha UVIKO-19. Na kwa kupitia sera na mikakati bunifu ambayo imesaidia shirika limeendelea kutoa huduma zake kwa ubora na kwa wakati pamoja na changamoto zilizojitokeza za ufinyu wa bajeti. Kupia mikakati hiyo Uongozi wa MHOLA uliweza kukutana na wadau kutoka taasisi mbalimbali ndani na nje; waliosaidia na kuongezea ujuzi na maarifa ambayo yaliwezesha kupata matokeo chanya katika malengo ya shirika. Tunaahidi kuendelea kutumia elimu, ujuzi na maarifa haya ndani na nje ya shirika kwa maendeleo ya baadaye.

MHOLA inatambua na kuheshimu ukweli kuwa uwepo wake unategemea na huduma bora inayotolewa kwa wateja (wapokea huduma) ambao ufika kuomba huduma na msaada wa kisheria. Kupitia kwao, taaluma na utendaji wa wafanyakazi uongezeka siku baada ya siku na wigo wa MHOLA kujitangaza unaongezeka. Tunawapongeza kwa kuendelea kutuamini na MHOLA tunaahidi kuendelea kutoa huduma zenye ubora kwa ajili ya maslahi yao.

MHOLA pia inawashukuru kwa dhati wafanyakazi wake wote waajiliwa, wanaojitolea na wanaofika kwa ajili ya kujifunza ambao wamekuwa sehemu kubwa ya mafanikio haya. Tunapongeza uvumilivu, utayari na kujitoa kwao hasa katika kipindi kigumu ambapo waliendelea kuheshimu matakwa ya mikataba yao, sera na kanuni za MHOLA.

Kwa ujumla, tunawaarika wote kuwa sehemu ya mpango wa MHOLA 2021/2022. Tuunganishe nguvu zetu katika kutumikia na kusaidia wenye uhitaji katika jamii. Tafadhari pitia malengo yetu na mipango yetu na kila mmoja awe huru kuona ni kwa namna gani anaweza kuwa sehemu ya mafanikio ya mipango yetu. Tuko tayari kupokea maoni yako kupitia tovuti yetu www.mhola.or.tz au kwa kutembelea ofisi zetu mahali zilipo.

## KUHUSU MHOLA

**Mamas' Hope Organization for Legal Assistance (MHOLA),** ni shirika lisilo la kiserikali na linalofanya kazi pasipokuzalisha faida ambalo limesajiliwa kisheria chini ya sheria ya Mashirika ya Kijamii (Cheti cha usajili Na. 14550), Sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 (Cheti cha Usajili Na. 00NGO00008006), chini ya Wizara ya katiba na sheria kama Mtoa huduma ya Msaada wa sheria (cheti cha usajili Na. LAP-2019-0005) na pia kusajiliwa kama mlipa kodi kupitia Namba ya Mlipa Kodi (TIN) 109-394-149. MHOLA imesajiliwa kufanya shughuli zake Tanzania bara lakini kutokana na upungufu wa rasilimali, inafanya shughuli zake katika kanda ya ziwa ususani mkoa wa Kagera.

MHOLA inanuia kuwa na jamii yenye afya ambayo haina umaskini wa kupindukia, ukatili wa kijinsia na ubaguzi. Haya yote yanaweza kufikiwa kupitia uwezeshaji wa jamii kwa kuwajengea uwezo kuhusu haki zao za msingi, mambo ya afya, utoaji wa msaada wa kisheria na msaada wa Kisaikologia (Huduma za kijamii) kwa wanawake na watoto na makundi maalumu ambayo hawana uwezo wa kufikia haki zao za msingi.

Mwaka wa fedha wa MHOLA uanza kila ifikapo Oktoba na kuisha Septemba ya kila mwaka, taarifa hii inahusisha kipindi cha Oktoba 2020 mpaka Septamba 2021. Kila mwaka MHOLA uweka malengo mahususi ili kufanikisha lengo kuu lililopo kwenye mpango mkakati wa miaka mitano (2019/2024) hivyo kwa kipindi hiki cha utekelezaji, MHOLA ilikuwa na malengo manne ambayo ni:

- **a.** Kuwawezesha wanawake na watoto kujua/kutambua haki zao msingi;
- **b.** Kukuza na kuendeleza swala la malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kwa maeneo ya pembezoni kwa kuongeza pato la kila kaya;
- **c.** Utoaji wa msaada wa kisheria na unasihi;
- **d.** Kujenga uwezo wa taasisi (MHOLA).

## MALENGO, SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA MAFANIKIO YAKE

**Lengo 1: Kuwawezesha wanawake na watoto kujua/kutambua haki zao za msingi**

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | UTEKELEZAJI ULIOFANYIKA |
|---|---|
| 1. Utoaji wa elimu ya sheria kwa watu 200,000 (60% wakiwa wanawake) ili kuongeza uelewa wa mambo ya kisheria na Malezi, Makuzi na Maendeleo ya mtoto. | Jumla ya watu **174,892 (94,626Me na 80,266Ke)** walifikiwa kupitia utoaji wa elimu. Wengi walifikiwa kwa njia ya maadhimisho ya wiki ya sheria, Siku ya Kimataifa ya wanawake, vipindi vya redio, vikundi vya kijamii na maadhimisho wa siku nyingine za kisheria na Kupitia mashindano ya ligi ya mpira maarufu MHOLA MIA MIA CUP<br><br>MHOLA pia ilitoa elimu ya sheria kwa wafungwa 1,301 (589Me na 712Ke) |
| 2. Kushiriki siku ya wazee duniani | Tarehe 15/06/2021 MHOLA ilishiriki kwenye shughuli iliyoandaliwa na shirika la Kwa Wazee ikilenga kutoa elimu kwa wazee 100 kutoka Kata ya Nshamba. Wakati wa utekelezaji halisi wazee hao 150 waliwezeshwa kuhusu unyanyasaji wa wazee na mambo mengine ya kisheria. |
| 3. Kuendesha mashindano ya Mpira wa Miguu (MHOLA Mia Mia Cup - 2021) | MHOLA iliweza kufikia zaidi ya watu 27,000 kutoka kwenye jamii ambao 80% walikuwa wanaume. Kupitia mashindano hayo, timu 16 kutoka wilaya ya Muleba, Bukoba Mkoani Kagera na timu 1 kutoka Mkoa wa Geita zilishiriki kwa kipindi cha mwezi mmoja. Lengo kuu ilikuwa kuhamasisha uandishi wa wosia. Hatima ya mashindano Timu kutoka Geita ilitwaa kombe. Baada ya ligi watu binafsi 204 (35% wakiwa wanawake) walifika katika ofisi za MHOLA na Paralegals kuomba ushauri/msaada zaidi katika uandishi wa wosia na usimamizi wa mirathi. |
| 4. Kuwajengea uwezo kuhusu mambo ya kisheria, Malezi makuzi na Maendeleo ya mtoto na shughuli za | MHOLA ilishiriki na kuwezesha warsha ya pamoja na wadau wa mahakama katika kutathmini miaka 100 ya utendaji wa |

| | |
|---|---|
| kujiongezea kipato | mahakama ambapo mapendekezo mbalimbali yalitolewa na wadau kwa ajili ya maboresho ya mahakama<br><br>Viongozi 30 watoa maamuzi walijengewa uwezo kuhusu haki za wanawake, watoto, haki ardhi, mirathi na malezi, makuzi na maendeleo ya watoto ili kuongeza weledi ktk utendakazi wao.<br><br>Aidha viongozi 40 wa vikundi vya kijamii walijengewa uwezo kupitia semina kuhusu shughuli za uzalishaji mali na pia kujikinga maambukizi ya virusi vya Homa kali ya UVIKO-***19***. |
| 5. Utoaji wa ruzuku kwa wasaidizi wa Kisheria na Vikundi vya kijamii | Mashirika 8 ya wasaidizi wa Kisheria mkoa wa Kagera yamepatiwa ruzuku kwa ajili ya kufanikisha shughuli za huduma ya msaada wa kisheria Zaidi ya millioni 16 zimetumika. |



Picha 2: Viongozi 30 wa Kijamii wakijengewa uwezo katika ukumbi wa MHOLA



Picha 3: Mashindano ya MHOLA Mia Mia Cup 2021 yakiendelea uwanja wa CCM Muleba

**Lengo 2: Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto kwa maeneo ya pembezoni na kuongeza pato la kaya**

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | UTEKELEZAJI ULIOFANYIKA |
|---|---|
| 1. Utoaji wa huduma ya Malezi ya watoto | Huduma ya malezi kwa watoto 35 imetolewa kituoni Muleba ambapo walipewa elimu ya |

| | |
|---|---|
| | darasani, kucheza, chakula na kupumzika kuanzia saa 3 asubuhi mpaka saa 9 mchana;<br><br>Walimu 7 kutoka MHOLA walihudhulia mafunzo jijini Mwanza kuhusu ufundishaji wa watoto wadogo kwa mtaala wa Montessori ambao unawapa uwezo wa kuandaa dhana za kufundishia na kufundisha pia. Mpaka sasa kituo kimeandaa dhana zake za kufundishia.<br>Kununua na kuweka dhana za kujifunzia na vifaa vya michezo kwa watoto kwa mujibu wa Mtaala wa Montesssori unaoongoza swala la malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. |
| **2.** Ukarabati wa majengo ya kituo cha malezi, madarasa na mazingira yake. | Ukarabati mkubwa umefanyika ambapo pia ujenzi wa chumba cha mapumziko na sehemu ya kulia chakula cha watoto. Majengo yote yamepakwa rangi upya kulinda uimara na kuongeza unadhifu. Ili kuongeza ulinzi, chumba cha mlinzi kimejengwa ili kufuatilia watu wote wanaoingia na kutoka kituoni. |
| **3.** Kuwezesha vikundi vya kijamii kwa kuwapa mbegu za kilimo na ujuzi wa uzalishaji mali | MHOLA imeendelea kutoa mbegu za pilipili na mihogo ili kusaidia jamii kuendeleza shughuli za kilimo.<br><br>Kutembelea vikundi na kuwajengea wanachama uwezo wa kusimamia fedha za mikopo wanayopokea. Matokeo ya utekelezaji huu asilimia kubwa ya vikundi wameongeza pato lao tofauti na hali waliyokuwa nayo awali. |
| 4. Ununuzi wa Pilipili kutoka vikundi vya kijamii | Mwaka huu, MHOLA ilinunua jumla ya kilo 500 za pilipili kutoka kwenye vikundi vya wakulima ambavyo vilisaidiwa elimu, mbegu na madawa kwa ajili ya kilimo cha pilipili kutoka MHOLA. |
| 5. Kuandaa na kushirikiana na wadau wengine wanajihusisha na malezi, makuzi na maendeleo ya watoto | Kituo cha MHOLA Day care centre kimetembelewa na wadau tofauti kutoka Ustawi wa Jamii, Idara ya Elimu, taasisi za serikali na binafsi.<br><br>Pia kituo kimetembelewa na wakufunzi wa Montessori kutoka Mwanza. |
| 6. Malipo ya ada za shule za wanafunzi | Katika kipindi cha mwaka wa utekelezaji, jumla ya watoto wanne wamesaidiwa ada za shule na mahitaji msingi ya elimu. |



***Picha 4. Afisa tathimini, Mkuu wa kitengo cha sheria kutoka MHOLA pamoja na Mwandishi wa Habari kutoka Kasibante FM walipotembelea kikundi cha WAWATA Bisore Kata ya Muhutwe Wilaya ya Muleba.***

**Lengo 3: Utoaji wa msaada wa kisheria na unasihi**

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | UTEKELEZAJI ULIOFANYIKA |
|---|---|
| 1. Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watu 3000 (30% wakiwa wanawake)- Huduma kwa mtu mmoja mmoja | Jumla ya watu 11,745 (5,298Me na 6,447Ke) walipata msaada wa kisheria ikiwemo ushauri, kuandaa nyaraka za kisheria, usuruhishi na uwakilishi mahakamani. 55% ya wanufaika ni wanawake. Aidha jumla ya kesi…………zilimalizika ambapo walengwa wetu waliopata ushindi…….walioshindwa ni…… |
| 2. Kutembelea na kuona utendaji katika wilaya za Muleba, Karagwe na Bukoba | Wilaya/Halmasahuri zote 8 za mkoa Kagera zimetembelewa. Uwezeshwaji katika ofisi ya Ngara na Bukoba umefanyika. Pia ofisi za Wasaidizi wa Sheria Bukoba, Karagwe na Ngara zimetembelewa na kuwezeshwa kiutendaji |
| 3. Ulipaji wa gharama zinazotokana na mashauri mahakamani | Wanufaika 53 wamepata msaada wa kulipiwa gharama za mahakama ikiwemo gharama za kulipa mahakamani, nauli na mahitaji mengine msingi wakati wa kuendesha kesi zao. |

| | |
|---|---|
| 4. Kulipa gharama za kuendesha mfumo wa utoaji wa msaada wa kisheria kwa njia ya mtandao na tovuti ya shirika | Tovuti na huduma za utoaji msaada kwa njia ya mtandao zilitoa huduma hadi kufikia July, 2021 ambapo mfumo ulifungwa kwa kuwa MHOLA haikuwa na pesa za kutosha kulipia mfumo huo. |
| 5. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utendaji za kila robo mwaka kuhusu utoaji wa msaada wa kisheria. | Taarifa zote za kiutendaji ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa wakati stahiki. |
|  **Picha 5**: Wafanyakazi wa MHOLA wakieleza shughuli za shirika kwa Mgeni rasmi katika wiki ya sheria, 2021 viwanja vya mahakama kuu Bukoba |  **Picha 6**: Utoaji wa msaada wa kisheria kwa wazee kwenye siku ya wazee duniani na kupinga ukatili dhidi ya wazee |

**Lengo 4: Kujenga uwezo wa taasisi (MHOLA**

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | UTEKELEZAJI ULIOFANYIKA |
|---|---|
| 1. Malipo ya kiutawala na uendeshaji wa ofisi | Malipo ya michango ya NSSF, Kodi ya mapato (PAYE), Mikopo ya elimu ya juu yalilipwa kila mwezi na kadri pesa ilivyopatikana. Ankala za maji, umeme ukarabati wa majengo na vifaa vya ofisi pia zililipwa. Hata hivyo katika kipindi cha Augosti- Decemba, hali ya kifedha kwa shirika haikuwa nzuri, hivyo baadhi ya wafanyakazi walifanya kazi kwa awamu ya siku 15 tu kwa mwezi. Pia mishahara ilisitishwa kipindi hicho. |
| 2. Utoaji wa vifaa vya kuzuia na kujikinga na UVIKO-19 | MHOLA iliweza kusambaza ndoo 200, boksi 200 za barakoa (za kitabibu), chupa 400 za sabuni ya kunawia mikono. Vifaa hivi |

| | |
|---|---|
| | viligawiwa kwa wasaidizi wa kisheria na wanachama wa vikundi vya kijamii. |
| 3. Safari za kiofisi na kuhudhuria mihariko | MHOLA ilipokea mialiko ya mikutano na Warsha mbalimabli zilizoandaliwa na Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Taasisi za Kidini. Mkurugenzi na Wafanyakazi wa MHOLA walipata fursa ya kuhudhuria, kutoa maoni na kujifunza pia. |
| 4. Harambee na Uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali. | Katika kipindi cha mwaka, tumeweza kuuza pilipili, kukodisha kumbi za mikutano na magari pamoja na kutoa huduma ya malazi kwenye nyumba za shirika. |
| 5. Kufanya ukaguzi wa miradi na matumizi ya fedha za shirika. | Kwa kipindi hiki, ukaguzi wa aina tatu umefanyia ambapo mmoja ulihusu matumizi ya fedha za shirika na nyingine mbili zilihusu miradi chini ya H3000 na LSF CFP05 |
| 6. Kufanya ufuatiliaji na Usimamizi wezeshi. | Kila robo mwaka ufuatiliaji umefanyika kwa ofisi za wasaidizi wa sheria, vikundi vya kijamii na matawi ya shirika.<br>Ufuatiliaji wa Kituo cha malezi Muleba umefanyika mara kwa mara kupitia Mkurugenzi na afisa Utuatiliaji na Tathimini wa shirika. |
| 7. Kuandaa na Kuwasilisha taarifa za utendaji kwa Wahisani (H3000) | Taarifa zote zinazohitajika kwa wahisani zimewasilishwa kwa wakati |




Picha 7: Afisa utuatiliaji na Tathmini wa MHOLA akitoa vifaa vya kupambana na UVIKO-19 kwa baadhi ya wanakikundi

**Shughuli ambazo hazikupangwa lakini zilifanyika**

| SHUGHULI | UTEKELEZAZI |
|---|---|
| 1. Msaada katika shuel ya sekondari ya Kiisilam ya Jakaya Kikwete | Jumla ya Tsh. 2,000,000/= (milioni Mbili tu) zilitolewa kwa shule ya sekondari ya Jakaya Kikwete –Muleba ili kununua magodoro baada ya kuungua kwa moto. Pesa hii ilikabidhiwa kwa mkuu wa Wilaya ya Muleba |
| 2. Mafunzo kwa wafanyakazi wa MHOLA kuhusu elimu ya uandaaji wa sera | Mafunzo yalifanyika chini ya ufadhiri wa H3000 ili kuwawezesha wafanyakazi kuandaa mijadara ya wazi ili kuibua matatizo yaliyopo kwenye jamii na kuhitaji kufanya mabadiliko ya sera |
|  **Picha 8: Mkurugenzi wa MHOLA akitoa kiasi cha Tsh. 2,000,000/= kwa mkuu wa Wilaya Muleba ili kununua Magodoro kwa ajili ya shule ya sekondari ya Jakaya Kikwete** |  **Picha 9: Wafanyakazi wa MHOLA wakishiriki mafunzo ya kuandaa mijadara ya wazi ili kuleta mabadiliko ya sera** |

## Vyanzo vya mapato

Kwa mwaka 2020/2021 kiasi cha ya **Tsh. 1,792,220,672.00** kilipangwa na shirika la MHOLA kuendesha shughuli za ofisi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa nia ya kufanikisha malengo ya shirika. Vyanzo vikuu vya mapato hayo ilikuwa kutoka kwa wafadhili waliokuwa wameonesha nia yao thabiti ya kusaidia shughuli hizi; Michango kutoka ktk jamii tunayoihudumia, aidha mapato ya ndani yatokanayo uzalishaji mdogomdogo wa shirika. Hata hivyo kiasi cha Tsh 427,501,805.25 tu ndo kilipatikana ktk kipindi cha mwaka mzima hii ni sawa na asilimia 25% ya makisio kwa mwaka husika. Hali hii iliathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa shughuli zilizokuwa zimepangwa

kufanyika na nyingine kutofanyika kabisa. Ikumbukwe janga la UVIKO-19 liliendelea kuzikumba nchi wafadhili na hivyo kujikuta wengi wao wakishindwa kuendelea kutoa ruzuku kama ambavyo waliahidi mwanzo.

## TULICHOJIFUNZA

Kupitia shughuli zote na mazingira ya kazi, tumejifunza kuwa:

a. Matumizi ya Mtandao kutoa huduma yalionekana kusaidia zaidi hasa kipindi cha UVIKO 19 ambako tulikuwa na wafanyakazi wachache lakini huduma kwa walengwa ziliendelea kutolewa hasa kutumia huduma mtandao.
b. Michezo hasa mpira wa miguu ni jukwaa muhimu na sahihi zaidi katika kufikia watu wengi katika utoaji wa elimu kwa jamii. Hii inaonekana wazi ambapo kupitia MHOLA Mia Mia cup zaidi ya watu 27,000 waliweza kufikiwa kwa muda mfupi.

c. Shughuli za MHOLA zinagusa maisha ya watu wengi na kusitisha huduma kunaathiri watu wengi. Hii imeonekana wazi kipindi hiki cha UVIKO-19 ambapo pamoja na kuhudumia wateja bure kwa njia ya mtandao, wengi walifika tena ofisini kwa maelezo zaidi. Kama ofisi zingefungwa basi wengi wangepoteza haki zao.
d. Vikundi vya kijamii pia ni jukwaa zuri zaidi kuwafikia watu wengi hasa wanaume ambao wao ndiyo watendaji na wavunjaji haki za wanawake na watoto kwa kiasi kikubwa.
e. Katika kipindi hiki cha utekelezaji MHOLA imepokea taarifa nyingi ya mauaji kwa wanaume, ambapo mauaji hayo yalichochewa na msongo wa mawazo kutokana na kushuka kwa kipato na migogoro sugu kati ya wanandoa.

## CHANGAMOTO

**1.** Kutokana na ufinyu wa bajeti huduma za msaada wa sheria kwa njia ya mtandao ulisitishwa kuanzia Julai 2021kwa kushindwa kulipia ada ya kila mwezi (airtime fee). Jambo, ambalo limepelekea watu waliopo mbali kushindwa kupata msaada wa kisheria kwa haraka au kukosa kabisa kupata huduma.

2. UVIKO-19 iliathiri kwa kiasi kikubwa mipango ya shirika kwani shughuli nyingi zilizokwama zinatengeneza kiini cha utendaji wa shirika. Aidha, pesa kidogo iliyopatikana ilielekezwa katika kukabiliana na Mlipuko wa UVIKO-19 kwa kununua vifaa vya kinga na ivyo kuathiri shughuli nyingine.
3. Wafadhili wengi walikumbwa na shida la UVIKO-19. Na hivyo kupelekea kushindwa kutoa ruzuku kama ilivyokusudiwa, aidha baadhi ya miradi ilifikia ukono mwaka jana na hivyo changamoto za UVIKO-19 zikapelekea wafadhili kushindwa kuendeleza/kutoa ruzuku mpya kama walivyokuwa wamehaidi mfano ni mradi ulikuwa ukifadhiliwa na mfuko Legal Service Facility. Ikumbukwe mradi huu ulikuwa unaghalimia shughuli nyingi za msaada wa kisheria ikiwemo kuwalipa wasaidizi wa kisheria.
4. Kutokana na uwepo wa UVIKO-19 vikundi vingi vya kijamii vinavyolelewa na kutunzwa na MHOLA vilipata hasara kwani uzalishaji ulipungua baada ya kufunga mipaka na kufanya biashara hasa ya mazao ya kilimo kuwa mbaya zaidi.

**MALENGO YA BAADAE (2021/2022)**

Pamoja na changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2020/2021, MHOLA bado tunayo nia thabiti yakufanya kazi na kuendelea kuitumikia jamii kwa kiwango kikubwa. Tukiongozwa na Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka mitano (2019/2024), tunayo nia kubwa ya kufanikisha malengo tuliyojiwekea na kadili mpango kazi unavyotuongoza hasa katika kukamilisha yale malengo manne ambayo ni:

a. Kuwawezesha wanawake na watoto kujua/kutambua haki zao msingi;

b. Kukuza na kuendeleza suala la Malezi, Makuzi na Maendeleo ya mtoto kwa maeneo ya pembezoni kwa kuongeza pato la kila kaya;

c. Utoaji wa msaada wa kisheria na unasihi;

d. Kujenga uwezo wa taasisi (MHOLA) kwa kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani.